HABARI KUHUSU KITOVU CHA KANADA CHA SHERIA ZA KIMATAIFA (CCIJ)

▶ CCIJ NI NINI?

Kitovu cha Kanada cha Sheria za Kimataifa ni shirika la taifa, la hisani, la haki za binadamu iliyo na makao Ottawa. CCIJ inafanya kazi na watu waliookoka kutoka kwa mauaji halaiki, mateso na madhuluma ili waweze kutafuta haki na kuwaadhibu waliotenda maovu haya. Sisi ni kikundi kilicho huru, kinachofanya bila mapato na hatuko pamoja na serekali la Kanada.

▶ NANI ANAWEZA KUFAIDIKA KUTOKA KWA HUDUMA ZA CCIJ?

Wateja wa CCIJ ni watu waliookoka mivunjo ya haki za binadamu au watu walio na uhusiano wa kabiru na wale waliokufa kwa sababu ya mivunjo yaa haki za binadamu au wale ambao wanashindwa kuwasiliana nasi.

▶ CCIJ INAFANYA NINI?

CCIJ ina madhumuni ya kuwa kitovu cha msaada kutoa habari kwa wateja wetu kuhusu hiari zao za njia tofauti ya kutafuta haki na kuwasaidia kupata njia zifaazo. Pia tunataka waliotenda mambo haya waadhibiwe kw matendo yao. CCIJ inapopata habari kuwa mvunja sheria ya haki za binadamu yupo Kanada au anahuzuru au ana uhusiano na shirika au kikundi iliyo hapa, tunaweza kuanzisha upelelezi. Mara nyingi, njia inayopendelewa ya hukuma ni kufanya kesi ya sheria kwa waliotenda maovu haya. Baada ya CCIJ kufanya mapelelezi ya mwanzo, kama mteja anapenda kufuatilia kesi au hatua nyingine, CCIJ itamrejea kwa mtu au ofisi inayofaa ili taratibu iweze kuendelea. CCIJ haitoi uwakilisho wa kisheria lakini inabaki ikishuguhulika na kesi yeyote na inamsindikiza mteja kwa mafuatano.

▶ KUNA AINA GANI ZA HAKI MTEJA ANAWEZA KUFUATILIA?

MASHTAKA YA UHALIFU KANADA NA NG'AMBO CCIJ inafanya mapelelezo yanayorejewa na serekali ya Kanada, nchi za kigeni au korti za kimataifa kwa mashataka ya wahalifu wa haki za binadamu. Kama upelelezi unafunua mathubuti wa kutosha na mteja anataka kufuatilia mashtaka ya uhalifu, tutawasiliana na afisa wanaofaa. Kama serekali au korti inataka kufuatilia mashtaka, CCIJ ita weka mteja katika uwasiliano na afisa na tutawapatia mathubuti tuliopata. Kesi hii inaporejewa kwa serekali au korti, tutaendelea kuhakikisha kuwa mashtaka yanafanywa katika njia taratibu na kwa haki na kutoa mapendekezo kwa washtaki inapotakikana.

MASHTAKA YA KIRAIA KANADA CCIJ inafanya mapelelezo yanayoweza kufuata uanzaji wa mashtaka yanayosababisha utafutaji wa malipo ya kusawazisha kwa wateja. Kama upelelezi unafunua mathubuti ya kutosha na mteja anataka kufuata na mashtaka ya kiraia, tutamsidia mteja kupata wakili atatakaye anza kesi bila malipo ya kisheria.

MARUDISHO CCIJ inatoa msaada kwa kesi za nchi geni au za kimataifa kwa kulingana na matakwa ya mteja au Kanada inapokataa au haiwezi kushtaki. CCIJ pia inasaidia kuwaleta wahalifu Kanada kwa mashtaka ya uhalifu nchi zingine zinapokataa au haziwezi kuchukua hatua.

KUONDOA UWENYEJI, UFUKUZO NA UTENGAJI CCIJ husaidia athabu ya majilio kwa wadhuluma wa haki za binadamu kama tu ndiyo suluhisho ya mwisho kama hakuna njia nyingine ya kuhukumu. CCIJ inapinga ufukuzo unaoweza kuongeza mivunjo ya haki za binadamu au kuwezesha wadhuluma kukwepa hukumu.

MALIPO YA KUSAWAZISHA KWA WATEJA CCIJ husaidia wateja wafuatilie malipo ya kusawazisha kwa kupitia mchango wa kusaidia wavumilizi.

JUHUDI ZA UWAZI/MATANGAZO CCIJ hufanya matangazo ili kuelimisha umma kuhusu matatizo na wadhuluma wa haki za binadamu walio Kanada.

CCIJ INAPELELEZA AINA GANI YA MADHULUMIO YA HAKI ZA BINADAMU?

Idadi kubwa ya mapelelezo ya CCIJ yanahusu watu ambao wameshtakiwa kwa kudhulumu haki za binadamu. Pia tunapeleleza dhuluma zinazofanywa na serekali za kigeni, serekali ya Kanada, mashirika, na vyama, kama vile vikundi vya wahalifu au askari.

CCIJ INAPELELEZA AINA GANI YA MIVUNJO YA HAKI ZA BINADAMU?

CCIJ haiwezi kupeleleza aina zote za uhalifu. Msaada wetu una kikomo na tunachagua kesi chache. Kesi za mivunjo ya haki za binadamu tunazopeleleza ni zile zinazodhaniwa na dunia kuwa ni kesi kali. Zinakadiriwa na matendo ya adhabu kali, hii inamaanisha kutendewa vibaya sana na afisa wa serekali, kwa kawaida mtu akiwa jela, au mauaji ya kisheria, inamaanisha mauaji yanayofanywa na afisa wa serekali. Kama mtu ni mtu aliyeokoka adhabu kali au mateso mengine makali zilizofanywa na afisa wa serekali, CCIJ inaweza kukusaidia umsaidie mtu huyo. Kama mtu ana uhusiano wa karibu na mtu ambaye aliyeuawa na serekali, askari, au kikundi cha wahalifu, CCIJ inaweza kukusaidia kuanzisha upelelezo.

MTEJA ANATAKIWA KUFANYA NINI KESI INAPOANZA?

Jukumu la mteja inategemea na aina ya kesi au hatua mteja ameamua kufuatilia. Kwa kesi zote, mteja atatakikiwa kupatia CCIJ habari ya kibinafsi na habari zaidi kuhusu hadithi ya mteja. Tunaelewa jinsi ni vigumu kuzungumza kuhusu matukio yenye kiwewe, kwa hivyo tutachukua utangulizi kutoka kwa mteja. Pia tunapendelea, ikiwezekana, kupata usaidizi kutoka kwa mteja ya kupata washahidi na mathubui. CCIJ ina sheria thabiti za kutunza faragha. Hatutoi kwa hiari yetu utambulisho wa wateja wetu, washahidi au tunaowasiliana nao au habari ya kisiri wanaotoa bila kutupatia idhini, ingawaje kuna nafasi ambapo korti inaweza kutuamrisha kufichua habari hii. Kama mteja anaamua kufuatilia mashtaka ya uhalifu, mashtaka ya kiraia au kesi yeyote ya kisheria, mteja bila shaka atatakikana kutoa ushahidi kortini mbele ya hakimu. Wakati mwingine inawezekana kuweka utambulisho wa mteja siri kutoka kwa umma, lakini mshtakiwa anayeshtakiwa katika kesi hiyo ana haki ya kujua majina ya washahidi wataotoa shuhuda.

WATEJA WANAPOKEA PESA KWA KUSHIRIKIANA NA KESI?

Kama mteja anafuata kesi ya kiraia au utaratibu wowote wa malipo ya kusawazisha, kuna uwezekano kuwa mteja anaweza kupata pesa lakini kufanya hivyo kutakuwa vigumu sana. Hakuna hakika kuwa mteja atapata malipo ya kusawazisha.

KESI INACHUKUA MUDA GANI?

Karibu kila kesi ya sheria inachukua muda mrefu kufika kikokmo. Upelelezi wa mwanzo wa CCIF unaweza uchukue miezi kadha au mwaka mmoja. Kuanzisha kesi kunahitaji miezi mingine zaidi. Kesi inapoanzishwa urefu wa utaratibu utategemea uwezo wa mshtakiwa kupinga kesi. Hata hivyo, kesi yeyote inaweza kuchukua muda usiopungua miaka mitatu au minne na inaweza kuchukua muda zaidi ya hiyo. Mteja bila shaka atafanya na CCIJ na wakili siku 10 kila mwaka, kutoa ushahidi, kusafiri kwenda kortini na kushirikiana na shughuli zinazo husiana na kesi. Hatua zingine zisizo za kesi za sheria zinahitaji muda kidogo.

JE MTEJA ANATAKIWA KULIPA PESA ILI UPELELEZI UANZE AU KUANZA KESI YA KISHERIA?

Hapana. CCIJ au wakili wengine au afisa wanaweza kulipa gharama zinazohusiana na upelelezi au kesi.

Kuzungumza na CCIJ, tafadhali wasiliana na afisa wa sheria Legal Coordinator, Matt Eisenbrandt:
Kwa simu: (613) 744-7667 ext. 266
Kwa emeli: meisenbrandt@ccij.ca
Kwa barua: 312 Laurier Avenue East
Ottawa, Ontario K1N 1H9

CCIJ

Dobrotvorni broj:
86575 9088 RR 0001

The Law Foundation of Ontario
Building a better foundation for justice in Ontario

Produced with support from
the Law Foundation of Ontario